## SEHEMU A

### Ama

**1. (a) Andika insha isiyopungua maneno 400 wala kuzidi 450 juu ya mojawapo ya mada zifuatazo;**

i) Serikali inafaa kuchukua hatua gani ili kudumisha Amani nchini mwako?

ii) Mitandao ya kijamii imesababisha madhara kuliko manufaa kwa wanafunzi. Jadili.

iii) Andika insha itakayoishia kwa '...............wenzangu,nilifikiri nilikuwa nimefika,kumbe sivyo."

iv) Kipendwacho na moyo ni dawa.

### AU

**(b) Andika insha mbili fupi kwa kuchagua miktadha miwili miongoni mwa hiyo hapo chini;**

i) Wewe kama mwalimu mkuu wa shule ya kutwa katika eneo lako,umeitisha mkutano wa wazazi ambao wamepata hofu kwamba watoto wao watatekwa nyara na mahaini barabarani wakiwa wanarudi nyumbani. Andika hotuba utakayowatolea kuhusu jinsi ya kuwalinda watoto wao dhidi ya watu hawa wenye nia mbaya.

*(Tumia maneno kati ya 180-200).*

ii) Andika ratiba itakayofuatwa wakati wa sherehe ya kuwatuza wanafunzi shuleni kwako waliofaulu katika mitihani yao ya kidato cha nne na wakapitia daraja la kwanza. *(Tumia maneno kati ya 100-150).*

iii) Watahiniwa wa kidato cha nne wamepatikana wamekiuka sheria ya shule ya kuvaa sare kamili ya shule.Wewe kama mwakilishi wa watahiniwa hawa umealikwa afisini mwa mwalimu msimamizi wa nidhamu. Andika mahojiano kati yako na mwalimu huyo. *(Tumia maneno kati ya 200-250).*

iv) Wanafunzi wa Kiswahili shuleni kwako wamezindua chama cha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mwalike mwalimu mlezi wa chama kwa ufunguzi rasmi wa mkutano wa chama hiki. *(Tumia maneno kati ya 50-60).*

*Uganda Certificate of Education*

**LUGHA YA KISWAHILI**

**Karatasi ya Kwanza**

**MUDA: SAA MBILI NA NUSU**

**MAAGIZO;**

- Jibu maswali **Manne.**
- Jibu maswali mawili mawili kutoka sehemu **A** na **B.**
- Swali la kwanza lina vipengele viwili. Chagua kipengele kimojawapo: **Ama (A) au (B).**
- Nadhifisha mwandiko wako.

**3. Soma Makala ifuatayo kisha ufupishe umuhimu wa Umuhimu wa viumbe kwa maneno yasiyozidi 100.**

Mwenyezi Mungu aliumba viumbe wengi sana duniani. Binadamu ndiye kiumbe mkuu wa viumbe wengine. Binadamu wa kwanza kuumbwa na Mungu ni Adamu na Hawa. Wanadamu hawa; Adamu na Hawa waliishi katika shamba la Edeni. Mungu aliwaambia watengeneze familia yao kwa kuzaa watoto, waijaze dunia nzima. Mungu aliwaambia kwamba kula tunda haramu ni dhambi au kosa kubwa. Lakini Adamu na Hawa walifanya makosa ya kula tunda haramu. Mungu alikasilika sana na kuwafukuza watu hao watoke kwenye shamba lake tukufu na kuwatupa hapa duniani. Maneno hayo yameandikwa katika Vitabu vitakatifu vya dini; Biblia ya wakristo na Korani ya waislamu.

Kuna viumbe wa aina nyingi duniani. Kwa mfano; wanyama, ndege na wadudu. Kuna Wanyama wa aina mbili; wanyama-pori na wanyama wanaofugwa nyumbani. Wanyama-pori wanakaa kwenye mbuga za wanyama misituni/porini/mwituni na majini. Wanyama wanaokaa misituni au porini ni kama vile; Simba, chui, Tumbili, Kifaru, swala, Nyati, Tembo, kuchakuro, Twiga, Pundamilia, Fisi, Mbweha, nakadhalika. Kwa nchi kama Uganda wanyamapori wanasaidia nchi kuingiza pesa za kigeni kutoka kwa watali wazungu. Pia kuna wanyama pori wanaokaa majini kama; Samaki, papa, Mamba na Kiboko.

Kuna wanyama wanaofugwa nyumbani kwa binadamu. Miongoni mwa wanyama wanaofugwa ni; Ng'ombe, Mbuzi, Mbwa, kondoo, punda, Ngamia, Nguruwe, Sungura , paka, panya na farasi. Wanyama hawa ni muhimu sana. Wanyama wanaleta faida kubwa mno kwa binadamu. Kwa mfano; Wanyama wanatupatia nyama ambayo ni chakula kwa binadamu, Wakulima wanapata pesa nyingi baada ya kuuza wanyama sokoni, wanyama wanafanya kazi kubwa ya kusafirisha watu na kubeba mizigo mizito, wanyama wanatupatia siagi na maziwa ya kunywa, Ngozi za wanyama zinasaidia binadamu kutengeneza viatu, ngoma, mikoba, nguo, kofia na silaha. Wanyama wanafanya kazi ya kulinda mali kama askari polisi nyumbani kwa binadamu.

Ndege au nyuni ni wa aina mbili; kuna ndege pori na ndege wanaofugwa nyumbani. Ndege wanaokaa porini au mwituni ni kama; Mbuni, kanga, korongo, Tausi, Kwale, tai, kipanga, Bundi, Mwewe na kadhalika. Ndege wanaofugwa nyumbani ni kama vile; Kuku, Bata, Kasuku, Batamzinga na Njiwa. Umuhimu wa ndege kwa binadamu ni kama; Kupata nyama ambayo ni chakula kwa binadamu, Ndege wanapatia binadamu mayai ya kula, Binadamu anapata pesa nyingi baada ya kuuza ndege, mayai na nyama ya ndege.

Viumbe wengine ni wadudu. Kuna wadudu wengi sana duniani kwa mfano; Mchwa, kumbikumbi, senene, panzi, kipepeo, kiwavi, siafu, sisimizi, kupe, funza, nyuki, Nzi, Mbu, Mende, mabuu, nakadhalika. Wadudu wana faida na *madhara chungu nzima.* Kwa upande wa mazuri (faida); Nyuki wanatengeneza asali ambayo ni tamu sana kwa binadamu, Wadudu ni chakula kwa binadamu. Wanadamu wengi wanakula wadudu kama vile; Kumbikumbi, mchwa na Senene. Kwa upande wa uhatari au mambo mabaya ya wadudu (madhara); wadudu wanasambaza ugonjwa kwa binadamu. Kwa mfano; Mbu wanasambaza ugonjwa wa malaria. Nzi wanasambaza

ugonjwa wa kipindupindu na waba. Wadudu wengine wanasumbua sana mwanadamu wanang'ata, wanauma, wanawasha na kuleta madhara na maumivu makubwa kwa mwili wa binadamu.

**4. Tafsiri ibara ifuatayo kwa Kiswahili sanifu;**

**HOW TALL WAS THE ROBBER?**

Mr Njau and Mr Okwata were two shopkeepers. They each had a shop in the centre of the town. The two men were very good friends. But people often laughed when they saw them walking down the road together, for while Mr Njau was exceptionally short, Mr Okwata was exceptionally tall. Mr Okwata was 195 cms tall, while his friend was only 135 cms.

One day, the two men were talking together when a white Peugeot 504 stopped on the other side of the street. The driver got out, and started to cross the street to buy a newspaper.

Suddenly, a stranger ran forward, and pulled out a pistol.

"Give me your car keys and your wallet!" he shouted, pointing the pistol at the driver's chest.

A few moments later, the thief drove away, leaving the driver standing in the road, too dazed to speak or move.

A few minutes later, Mr Njau and Mr Okwata went to the police station to help the police with their enquiries. The driver went with them. At the police station Sergeant Odinga showed them into his office.

"The robber was very short...." Began Mr. Okwata.

"No, he wasn't he was tall!" interrupted Mr Njau.

"What do you say?" asked the Sergeant, looking at the driver. But he was still suffering from shock.

"I-I can't remember!" he said. Sergeant Odinga looked from one to the other. Just then inspector Kahara walked in. At first he listened to the argument for a few minutes, and then called for silence.

" I think I can solve this problem," he began. "It is clear that in comparison with Mr Njau the robber was tall. But in comparison with Mr Okwata, he was short. Can we agree therefore that as one of you is very tall, and the other very short, the wanted man is probably of average height?"

The two friends were delighted at this simple solution.

**5. MATUMIZI YA LUGHA**

a) Tumia neno lenye maana sawa na yaliyoelezwa katika sentensi hapo chini.

i) Mimi ni sehemu katika jangwa ambapo unaweza kupata maji.(alama 02)
ii) Maji yaliyoganda na kuwa jiwe jeupe. (alama 02)

b) Geuza sentensi hizi ziwe katika umoja.

na kumuondoa pale hadharani.Wanafunzi na walimu walijaribu kumpa huduma ya kwanza lakini hawakufua dafu,kwani Mwafia hakuamka.Punde wanafunzi walikumbuka ya kwamba Mwafia ana "dawa"yake ambayo hubugia mara kwa mara. Hivyo basi mmoja wa maarifu wake alimita mwanafunzi mmoja kando na kwa siri akampa "unga" mchache.Mwanafunzi huyo alimpelekea Mwafia na kumnusisha bila ya walimu kuona. Mara tu Mwafia alipounusa "unga" ule alifungua macho na kutabasamu.Alipoanza kupata fahamu vizuri walimpa ule uliobaki akaubugia na kisha akaamka. Hivyo ndivyo ilivyokuwa mara ya mwisho kwa Mwafia kuonekana shuleni.

**Maswali**

a) Taja sababu mbili zilizowafanya wanafunzi kunadhifisha kila mahali shuleni. (alama 02)

b) Eleza jukumu la Mwalimu mwongoza tamasha anayetajwa na mwandishi (alama 01 )

ch) Mwafia alipatwa na shida gani alipokuwa jukwaani? (alama 02)

d) Tambua sifa zezote nne za Mwafia (Alama 02 )

e) Kutokana na maelezo yako mwenyewe,unga aliopewa Mwafia ulikuwa unga gani? (Alama 01)

f) Kwa nini dawa aliyopewa Mwafia ilitolewa kwa siri bila kuonyeshwa kwa walimu? (alama 02)

g) Mwandishi ana maana gani anaposema,...hata yale magofu yaliyokuwa yamesahauliwa miaka nenda miaka rudi,' ( alama02)

h) Kwa nini mwandishi alilinganisha ziara hii kwa ile ya kumtarajia Malkia? (alama02)

i) Toa sababu iliyowatamanisha wanafunzi kuwa na siku ya wazazi kila mwezi? (alama 02)

h) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika ibara.

i) ng'ara (alama01)

ii) mtanashati ( alama01)

iii) kufumba na kufumbua (alama01)

iv) hawakufua dafu (alama01)

**2. Soma ibara ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata.**

Siku moja wakati wa siku ya wazazi shuleni kwetu tulishuhudia kisa cha kunuzunisha sana. Siku hiyo kila mwanafunzi aliamka mapema akiwa na furaha na bashasha ya kukutana na mzazi wake au mlezi wake.

Basi kama ilivyo kawaida,wanafunzi walianza kufagia na kuokota makaratasi kwani tayari sehemu nyingi za shule zilikuwa zimenadhifishwa awali. Shule ilikuwa ni safi,inang'ara kwani majengo yote yalikuwa yameshapakwa rangi ya maziwa na kupigwa mkato wa rangi ya kahawia. Njia zote zilikuwa zimepangwa mawe ambayo yalirashiwa na kupulizwa chokaa nyeupe. Miti nayo haikusahaulika,ilipakwa rangi nyeupe mle mashinani.Nyasi zilikatwa kwa urefu wa kimo cha nyoka na bustani kusawazishwa. Alimradi kila mahali palionekana pamwng'ara jinsi shule ilivyopambwa na kurembeshwa ungefikiri tulimtarajia Malkia kuzuru shule yetu.kwani hata yale magofu yaliyokuwa yamesahauliwa miaka nenda miaka rudi pia yalipakwa rangi baada ya kufanyiwa ukarabati.Walimu na wanafunzi walistaajabu, 'lo! Na pesa zote hizi zimetoka wapi?'

Baadaye wageni,wazazi,ndugu na marafiki walianza kuwasili na mwongoza tamasha ambaye alikuwa mwalimu wetu wa Kiswahili akatushauri tukusanyike mahali pamoja kupitia kwa kipaza sauti. Baadhi ya wageni walikuwa wamefika na kukaribishwa kwenye ukumbi ambao pia ulikuwa umejengwa mahsusi kwa sherehe hiyo.

Kipindi cha kuwatumbuiza wazazi na wageni kiliwadia. Tukajipanga kulingana na ratiba iliyotayarishwa awali.Vikundi vya awali vikatangulia kisha zamu ya Mwafia ikafika. Mwafia alikuwa kijana shupavu na mwerevu darasani lakini alikuwa hana afya nzuri na mara nyingi akivaa nguo chafu na kuchana kwa nadra nywele zake ndefu za kipilipili. Lakini ajabu siku hiyo alionekana mtanashati. Nywele zake kanyoa,zikawa fupi na nzuri.Alivaa sare mpya ya shule,akafunga tai na akavaa koti. Viatu viling'ara kushinda vya wanafunzi wengine wote.Wengine walisikika wakisema,Huyu si yule Mwafia tumjuaye! Lakini kama itakuwa hivi,siku za wazazi zije kila mwezi.

Japokuwa Mwafia aling'ara sana siku hiyo,afya yake ilikuwa bado ina dosari.Mwafia alipanda jukwaani ili kukariri shairi lake juu ya mahitaji ya wanafunzi shuleni.kufumba na kufumbua watu walimuona Mwafia amelegea na kuanguka chini kama gunia shinda huku akiweweseka na kuanza kuita "Nyundooooo,Nyundoooo,Nyundoooo,...."Wanafunzi wenzake walimkimbilia

i) Madhumuni yetu yamefikiwa vikaoni. (alama 02)
ii) Tulitarajia maelezo yafaayo kutoka kwa walimu. (alama02)

Ch) Jibu kila swali ukifuata maagizo yaliyotolewa katika mabano bila kubadili maana;
i) Amesifiwa kwa uadilifu wake.(andika bila kwa) (alama 02)
ii) Abiria walipata ajali ***mahali ambapobarabara zinakutania***. (tumia neno moja kuwasilisha maneno katika herufi zilizokolezwa). (alama 02)

d) Geuza kwa kauli ya kutendwa ;
i) Wahalifu huteka watu nyara nakudai jamaa zao pesa nyingi (alama 02)
ii) Hesabu hizi zilinifikirisha sana. (alama 02)

e) Tunga sentensi ukitumia vihisishi vifuatavyo:
i) Yarabi! (alama 02)
ii) Ala! (alama 02)

f) Kamilisha tashibibihi hizi;
i) laini kama................................................ (alama 02)
ii) Mkaidi kama.............................................. (alama 02)

g) Toa maana ili kutofautisha kila jozi la maneno yalipewa chini;
i) Macheo, Machweo (alama 02)
ii) Futa, Vuta (alama 02)

h) Andika kwa usemi wa taarifa:
i) 'Oh! Umerudi haraka mwanangu,"mama alisema, 'umefanikiwa?"(alama 02)
ii) 'Mauaji ya watu yamezidi mno nchini!" Mwananchi alilalamika. (alama 02)

i) Sahihisha sentensi kwa Kiswahili sanifu;
i) Mahali mwenye uchafu kulifagiliwa. (alama 02)
ii) Makati tuliwasili tulikuta mgeni akesha ondoka. (alama 02)

j) Eleza maana ya methali hizi.
i) Acheleaye mwana kulia hulia mwenyewe. (alama 02)
ii) Mwenye pupa hadiriki kula utamu. (alama 02)

**MWISHO**